BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA BAJETI KUHUSU MKABALA WA BAJETI, UCHUMI NA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2019/20-2021/22

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na uzima nikaweza kwa mara nyengine kusimama mbele ya Baraza hili tukufu nikiwa na nguvu za kutekeleza majukumu yangu. Aidha, nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa lengo la kutoa maoni ya Kamati ya Bajeti juu ya Mapendekezo ya Mkabala wa Bajeti, Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2019/20-2021/22.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru kwa dhati watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Ndg. Khamis Mussa kwa kufika mbele ya Kamati na kuwapatia ufafanuzi Wajumbe juu ya masuali mbali mbali ambayo walihitaji kupatiwa ufafanuzi kuhusiana na waraka uliowasilishwa.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nichukue fursa hii pia kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bajeti ambao kwa umakini mkubwa wameupitia waraka huu wa Mkabala wa Bajeti na kutoa maoni na ushauri kwa lengo la kuongeza ubora katika Bajeti na Mipango ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, nawashukuru Makatibu wa Kamati ya Bajeti kwa kutekeleza vyema majukumu yao ya kuwashauri Wajumbe pamoja na kuratibu shughuli mbali mbali za Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba niwatambue kwa majina Wajumbe na Makatibu wa Kamati kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mohamed Said Mohamed | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Bahati Khamis Kombo | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Asha Abdalla Mussa | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Abdalla Ali Kombo | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Simai Mohammed Said | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Abdalla Ali Shauri | Katibu |
| 9. | Ndg. Asha Said Mohamed | Katibu |
| 10. | Ndg. Kassim Tafana Kassim | Katibu |
| 11. | Ndg. Shaib Fadhil Shaib | Katibu |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti imetimiza masharti ya Kanuni ya 92 (3) na 92 (4) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2016, yanayoelekeza kupokea Muelekeo wa Mpango wa Taifa na kuutolea maoni. Kwa ruhusa yako **Mheshimiwa Spika**, naomba niwasilishe maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusiana na waraka huu ambao umegusia Mapitio ya Hali ya Uchumi na Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2017/2018, Mapitio ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Utekelezaji wa Bajeti (2018/2019) kwa kipindi cha miezi sita kinachoishia tarehe 31 Disemba na Matarajio ya Ukusanyaji wa Mapato na Matumizi ya Serikali hadi Juni 2019 na Mapendekezo ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha miaka mitatu 2019/2020-2021/22.

## MAPITIO YA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** takwimu zilizowasilishwa katika waraka wa Mkabala zinaonesha kuwa Zanzibar inaongoza kuwa na ukuaji mzuri wa uchumi, kwa kuwa na kasi ya ukuaji wa uchumi wa asilimia 7.7 kulinganisha na nchi nyingi za ukanda wa Afrika ya Mashariki, kulikochangiwa na sababu mbali mbali ikiwemo kuongezeka kwa uzalishaji wa zao la karafuu kufikia tani 4,679 zenye thamani ya TZS 65.6 bilioni mwaka 2016.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mchango wake mkubwa katika uchumi, biashara ya zao la karafuu inakabiliwa na changamoto ya

kuathiriwa na hali ya hewa na misimu ya mavuno, ambapo katika msimu mdogo wa mavuno ya zao hilo, mauzo ya karafuu hushuka sana kiasi cha kuongeza nakisi ya biashara za nje. Kwa lengo la kuufanya mchango wa zao la karafuu kuwa endelevu katika ukuaji wa uchumi, Kamati inaishauri Serikali, kutanua wigo wa biashara kwa kuanza utaratibu wa kulisarifu zao la karafuu na kuuza bidhaa zinazotokana na zao hilo, ambazo mauzo yake hayataathiriwi kwa kiasi kikubwa na misimu ya mavuno kama ilivyo sasa.

**Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kuimarika kwa hali ya uchumi wa Zanzibar kupitia pato la kila mtu ambalo linaonekana kukuwa kwa kasi ya wastani wa asilimia 11.3 pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula kwa kiasi kikubwa katika mwaka 2017. Hali halisi kwa maisha ya wananchi ni tofauti na takwimu hizo, kutokana na kuongezeka kwa ugumu wa maisha ya mwananchi mmoja mmoja. Kamati inaishauri Serikali, katika bajeti ya mwaka wa fedha wa 2019/2020, kuweka mikakati madhubuti itakayo hakikisha takwimu za ukuaji wa uchumi zinaakisi hali halisi ya maisha ya wananchi ili dhana ya bajeti ya wananchi iweze kufikiwa.

## UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA PROGRAMU NA MIRADI KWA KIPINDI CHA JULAI – DISEMBA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa

mwaka 2018/2019 ulijumuisha Programu 27 na Miradi 55 ambayo ilipangiwa Jumla ya TZS 613 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo kwa mwaka huo wa fedha. Kwa kulinganisha Bajeti ya maendeleo ya mwaka 2017/2018 iliyotengewa jumla ya TZS 496.6 bilioni na bajeti ya maendeleo ya mwaka 2018/2019 iliyotengewa jumla ya TZS 613 bilioni kuna ongezeko la TZS 116.4 bilioni kwa bajeti ya 2018/19 katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo**.** Pamoja na ongezeko hilo, Kamati haijaridhishwa na mchango wa Serikali katika bajeti ya maendeleo, kwa kuwa mchango wake bado ni mdogo ambao ni TZS 148.8 bilioni ukilinganisha na mchango unaotokana na mikopo na ruzuku kutoka nje ambao umekadiriwa kuwa TZS 464.2 bilioni.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2018/2019 umebakia muda mfupi kabla ya kumalizika na kwa kuwa kuna miradi muhimu kama mradi wa kuendeleza Bandari ya Mangapwani, ujenzi wa barabara ya Chake Chake - Wete na ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri, hakuna fedha iliyoingizwa kwa ajili ya utekelezaji wake, Kamati inasisitiza upatikanaji wa fedha kwa ajili miradi hiyo kwa kipindi kilichobakia ili utekelezaji wa miradi hiyo iweze kufanyika sambamba na kupangiwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti ijayo ya mwaka 2019/2020.

**UTEKELEZAJI WA MIRADI KWA MAENEO YA VIPAUMBELE KWA KIPINDI CHA JULAI – DISEMBA, 2018**

**Mheshimiwa Spika,** waraka wa Mapendekezo ya Mkabala wa Bajeti, Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2019/20 -2021/22 unaeleza utekelezaji wa miradi kwa maeneo ya vipaumbele kwa kipindi cha Julai - Disemba, 2018 kuwa ni pamoja na kuimarisha miundombinu ya maeneo ya uingiaji nchini. Kamati imebaini kuwa, baadhi ya maeneo ya vipaumbele kwa mwaka 2018/2019 ikiwemo ujenzi wa Jengo la Abiria la Uwanja wa Ndege wa Zanzibar (Terminal III) bado utekelezaji wake hauja kamilishwa kama ulivyoainishwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia umuhimu wa utekelezaji wa vipaumbele katika miradi ya maendeleo, na kwa kuwa Kamati haikuridhishwa na maelezo ya utekelezaji wa miradi kwa baadhi ya maeneo ikiwemo maeneo ya kuimarisha miundombinu ya uingiaji nchini, maeneo ya kuendeleza utalii na maeneo ya kuimarisha viwanda vidogo vidogo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa vipaumbele vinavyoainishwa kupitia bajeti vinatekelezwa ipasavyo na pia Serikali kuendelea kusimamia Wizara na Taasisi zake kwa kuhakikisha kuwa, maeneo yanayoainishwa katika bajeti yanafanyiwa kazi kwa wakati na kuondosha kasoro mbali mbali ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa bajeti.

## MFUKO WA MIUNDOMBINU

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mapato ya Mfuko wa miundombinu, jumla ya TZS 39.5 bilioni zilikadiriwa kukusanywa na kwa kipindi cha Julai - Disemba 2018, mapato yaliyopatikana yamefikia TZS 16.1 bilioni sawa na asilimia 40.8 ya bajeti ya mwaka mzima. Kwa kuwa matumizi ya mfuko wa miundombinu yanahusisha kuimarisha shughuli za miundombinu pekee na kwa kuwa mapato ya mfuko yalifikia asilimia 40.8. Kamati inaitaka Wizara ibainishe matumizi halisi ya mfuko yaliyokusudiwa kwa mujibu wa Sheria, kwa kuwa katika nchi yetu bado kuna changamoto nyingi za miundombinu ya barabara hususani katika maeneo ya uwekezaji licha ya kuwa fedha za mfuko huo zinaripotiwa kuongezeka.

## DENI LA TAIFA

**Mheshimiwa Spika,** Deni la Taifa limeongezeka kutoka TZS 391.8 bilioni Disemba 2017 mpaka kufikia TZS 779.4 bilioni Disemba 2018 sawa na ongezeko la asilimia 99. Kwa kuwa deni linaongezeka kwa kiwango kikubwa. Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya uhimilivu wa Deni (Debt Sustainability Analysis) kila baada ya muda, ili kupima hali ya deni na uhimilivu wake kwa kipindi cha muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu na kuweza kufahamu kwa kina namna ya ukuaji wa deni hilo na hali ya uchumi wetu. Aidha, Kamati inapendekeza wakati Serikali inapotoa taarifa za deni la taifa

kuonesha kiwango cha deni kilicholipwa na pia kubainisha mashirika au nchi zinazotudai.

## MATARAJIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

### Matarajio ya Mapato

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo wa makusanyo ya mapato katika kipindi cha Julai – Disemba 2018 unaonesha mapato ya mwaka wa fedha 2018/2019 yanatarajiwa kufikia jumla ya TZS 1.1 trilioni ikiwa ni sawa na ukuaji wa asilimia 20.9 ikilinganishwa na mapato ya TZS 909 bilioni ambayo yamekusanywa kwa mwaka wa fedha uliopita. Aidha, kwa upande wa mapato ya ndani yanatarajiwa kufikia jumla ya ya TZS 803.6 bilioni sawa na asilimia 73.1 ya mapato yote na mapato ya nje yanatarajiwa kufikia jumla ya 295.8 bilioni ambayo sawa na asilimia 26.9.

### Matarajio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2018/2019, matarajio ya matumizi ya Serikali yanatarajiwa kufikia TZS 1.1 trilioni sawa na ongezeko la asilimia 20.9 ya matumizi ya mwaka wa fedha uliopita ambayo yalikuwa TZS 899.5 bilioni. Matumizi ya kazi za kawaida yanatarajiwa kufikia TZS 721.8 bilioni sawa na asilimia 65.7 ya jumla ya matumizi na kwa upande wa matumizi ya Kazi za Maendeleo ni

377.6 bilioni ambayo sawa na asilimia 34.3 ya matumizi yote kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** matumizi ya mishahara (Ruzuku) ni TZS. 109.3 bilioni wakati katika bajeti zilitengwa TZS.104.6 sawa na ongezeko la TZS. 4.7 bilioni. Kwa Matumizi Mengineyo ni TZS.148.6 bilioni lakini katika bajeti zilitengwa TZS.147.3 bilioni, ambayo inafanya kuwe na ongezeko la TZS.1.3 bilioni. Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali ni TZS.148.5 bilioni, wakati katika bajeti zilitengwa TZS. 132.8 bilioni sawa na ongezeko la TZS.15.7 bilioni. Hivyo, jumla ya ongezeko linakuwa TZS. 21.7 bilioni. Kamati inaisisitiza Serikali kufanya uchambuzi wa kina wakati inapofanya makadirio ya matumizi ili kuepusha ongezeko kubwa la matumizi na kuathiri utekelezaji wa shughuli nyengine muhimu.

## MWELEKEO WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

### Majukwaa ya Bajeti na Uchumi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefarijika sana na hatua za Wizara ya Fedha na Mipango ya kuanzisha majukwaa ya Bajeti na Uchumi kama ilivyoelekezwa na Sheria ya Fedha Nam. 12 ya 2016 kifungu namba

38 na kifungu 87(1). Kamati inaamini kuanzishwa kwa majukwaa hayo, kutatoa fursa zaidi ya ushirikishwaji  wa wananchi katika matayarisho ya bajeti kwani ni muhimu kwa bajeti kuwa na mahusiano na sera pamoja na ushirikishwaji wa Umma.

## MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO 2019/2020 – 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** lengo la Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020 ni kuifanya Zanzibar kuwa nchi ya uchumi wa kati na kuondosha kabisa umaskini. Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ni mpango wa muda mrefu wa maendeleo ya uchumi wa jamii. Kwa kuwa imebaki miezi michache kufikia tamati ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020, Kamati inaishauri Serikali kutoa taarifa ya kina ya malengo (goals) ya Dira kwa kuainisha viashiria (indicators) na matokeo (outcomes) yaliyofikiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapendekeza kutolewa ufafanuzi wa utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa katika mwaka wa fedha uliopita. Ufafanuzi huo utaje vipaumbele, viashiria vyake na malengo yake. Aidha, Kamati inashauri kuwepo muendelezo wa vipaumbele ambavyo utekelezaji wake haujakamilika, kwani bajeti ni kioo cha mapato na matumizi kinachoonesha maeneo ambayo Serikali inayapa kipaumbele.

## MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Mapendekezo ya Mkabala inaonyesha kuwa Zanzibar inaweza kuongeza ukuaji wa uchumi na kuwa nchi ya kipato cha kati na kuimarisha ustawi na maisha ya Wazanzibari iwapo yatafanyiwa kazi zaidi maeneo manne ambayo ni vichocheo vya ukuaji wa uchumi wa Zanzibar. Maeneo hayo ni Uchumi wa Bahari (Blue Economy), Sera ya Viwanda ya Zanzibar, Sekta ya Utalii na Viwanda vidogo vidogo.

**Mheshimiwa Spika,** maeneo ambayo yameainishwa kama ni vichocheo vya ukuaji wa uchumi wa Zanzibar, mafanikio ya utekelezaji wake kwa kiasi kikubwa yanategemea ushiriki wa sekta binafsi. Hivyo, ili kupata muitikio mzuri wa sekta hiyo, Kamati inaishauri Serikali wakati wa kuandaa mikakati ya kuendeleza maeneo hayo, izingatie kuzitatua changamoto zinazowakwaza wawekezaji ikiwemo changamoto za kodi, masoko pamoja na changamoto za kiutawala zinazohusu taratibu za uwekezaji, kwani changamoto hizo zinaweza kuwa ni sababu ya kuzorotesha uwekezaji na hivyo kupelekea kutofikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya 2020 ya kuwa nchi ya kipato cha kati (Middle income country).

**Mheshimiwa Spika,** ili kutanua wigo wa ushirikishwaji wa sekta binafsi katika shughuli za uchumi, Kamati inaishauri Serikali katika

ziara za nje za viongozi wakuu zinazohusu masuala ya uchumi na biashara, iwashirikishe wafanyabiashara kwa baadhi ya ziara hizo. Hatua hiyo itawasaidia wafanyabiashara kujifunza na kuibua fursa mpya za biashara ambazo wanaweza kuzitumia katika kuendeleza uchumi wa nchi yetu. **Mheshimiwa Spika,** tumekuwa tukishuhudia viongozi wa nchi nyingi wanaambatana na wafanyabishara wakubwa katika ziara zao. Hivyo, si vibaya na Zanzibar tukaiga jambo hilo ambalo tunaamini litaleta tija kwa wafanyabiashara wa Zanzibar.

## PATO LA TAIFA

**Mheshimiwa Spika,** Pato halisi la Taifa kwa mwaka 2019/20 linatarajiwa kukua kwa kasi ya wastani wa asilimia 7.8. Matarajio ya ukuaji wa Pato la Taifa yatachangiwa na kuimarika kwa sekta ndogo ya usafirishaji, kilimo na ufugaji, biashara ya zao la karafuu, kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta ya utalii, kuimarika kwa fursa za uchumi wa bahari na kupungua vikwazo vya kufanya biashara Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa ya asilimia 7.8 inayotarajiwa kufikiwa mwaka 2019/20 ni kubwa na kimsingi ni hatua nzuri ya mafanikio ya kiuchumi. Hata hivyo, ikilinganishwa na kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa iliyokadiriwa kwa mwaka 2018/19 ya 7.7 utabaini kuwa, kuna ongezeko dogo sana la asilimia 0.1 tu. Hii inaonesha kuwa bado juhudi zaidi zinapaswa kuchukuliwa ili tuweze

kufikia malengo ya kuwa na ukuaji wa uchumi wa asilimia 8 hadi 10 kwa kipindi cha mwaka 2019/20-2020/21.

**Mheshimiwa Spika,** kuongezeka kwa Pato la Taifa ni moja kati ya viashiria vya uchumi mzuri katika nchi. Hivyo, kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa inapaswa pia iende sambamba na uimarishaji wa hali ya kipato cha mwananchi, uimara wa fedha ya ndani na udhibiti wa Mfumko wa Bei. Aidha, Kamati inaishauri Serikali iwahamasishe wananchi kuzitumia fursa za kiuchumi hususani katika sekta ambazo zinakuwa kwa kasi zaidi na wananchi hawajazitumia ipaswavyo ikiwemo sekta ya Utalii na Ujenzi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefarajika kuwa, miongoni mwa sekta zinazotarajiwa kuimarika kwa mwaka 2019/2020 ni pamoja na sekta ya kilimo, ambayo athari ya ukuaji wake inamgusa mwananchi moja kwa moja. Aidha, kuimarika kwa sekta hiyo kutapelekea kupunguza kasi ya uagizaji wa bidhaa za chakula nje ya Zanzibar ambazo zimekuwa na mchango mkubwa katika kupandisha kasi ya mfumko wa bei na hivyo kupelekea kupunguza uwezo wa manunuzi (purchasing power).

## SURA YA BAJETI

### Mwelekeo wa Mapato

**Mheshimiwa Spika,** mapato ya Serikali kwa mwaka 2019/2020 yanatarajiwa kufikia TZS 1.5 trilioni. Kamati inapongeza sana juhudi zinazochukuliwa na Serikali za kuongeza ukusanyaji wa Mapato, hatua ambayo bila shaka itaongeza ufanisi wa utekelezaji wa Bajeti na kupunguza utegemezi wa fedha za nje ambazo kukosekana kwake imekua ni sababu kubwa ya utekekelezaji usioridhisha wa Bajeti hususani kwa miradi ya maendeleo. Kamati inaishauri Serikali kuendelea na mikakati ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato kwa kuziba mianya ya uvujaji wa mapato sambamba na kutanua wigo wa ukusanyaji wa mapato kwa kuvifikia vianzio ambavyo bado havijaanza kukusanywa hususani katika sekta isiyo rasmi.

**Mheshimiwa Spika,** kuwatambua wafanyabiashara wa sekta isiyo rasmi sio tu itasadia kupata mapato lakini pia itasaidia kuwa na takwimu sahihi za shughuli za uchumi na mzunguuko wa fedha kwa ujumla.

**Mwelekeo wa Matumizi**

**Mheshimiwa Spika,** matumizi ya Serikali Serikali kwa mwaka 2019/2020 yanatarajiwa kufikia TZS 1.5 trilioni. **Mheshimiwa Spika,** Kamati inasisitiza wakati matumizi ya Serikali yakiongezeka, matumizi hayo yaende sambamba na hatua za udhibiti wa matumizi kwa kuhakikisha kunakuwepo na nidhamu ya matumizi ya fedha za umma na kuepuka matumizi yasiyo ya msingi. Maafisa masuuli

(Accounting Officers) wanaokabidhiwa fedha hizo pamoja na vyombo vya ukaguzi vinatakiwa kwa pamoja kufanya kazi kwa misingi ya uadilifu na uwajibikaji pamoja na kuzingatia taratibu za Sheria za fedha na manunuzi, ili faida za ongezeko la matumzi hayo ziwafikie wananchi.

**HITIMISHO:**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia naomba kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Mapendekezo ya Mkabala wa Bajeti, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa mwaka 2019/2020 hadi 2021/2022. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe kwa kunisikiliza. Nawaomba wayachangie mapendekezo haya na kutoa maoni yao ili yaweze kuzingatiwa katika matayarisho ya bajeti ya mwaka 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Mohamed Said Mohamed,

..........................................

Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**